

Noaks Ark

Noaks Ark inajitahidi kupunguza maambukizi ya VVU na majongwa mengine ya zinaa. Tunasaidia watu wanaoishi na VVU pamoja na watu wao wa karibu. Vilevile tunatoa huduma za elimu, habari pamoja na ushauri nasaha. Tunatoa huduma ya vipimo vya VVU kwa haraka, tunatoa msaada kwa waathirika pamoja na kuandaa shughuli za kijamii. Tafadhali wasiliana nasi!

Unga mkono kazi zetu – kuwa mwanachama

www.noaksark.org/medlem

Swahili



Noaks Ark hupatikana hapa

Luleå simu: 0920-23 06 50

Umeå simu: 076-776 18 88

Sundsvall simu: 070-239 39 65, 076-298 01 60

Gävle simu: 026-18 33 01

Stockholm* simu: 08-700 46 00

Norrköping* simu: 011-443 37 00

Växjö* simu: 0470-193 81

Göteborg simu: 031-361 46 00

Malmö* simu. 040-611 52 15

www.noaksark.org/vi-finns-har

* Au kliniki zenye vipimo vya VVU kwa haraka (majibu baada ya dakika 15)

Utajuaje iwapo una maambukizi ya VVU?

Njia pekee ya kufahamu ni kupima VVU. Vipimo hivyo huwa ni vya bure na unaweza kupimwa pasipo kujulikana jina lako. Unaweza kupimwa kwetu Noaks Ark na kwenye kliniki za magonjwa ya maambukizi, “Sesam clinics”, kliniki za vijana, kliniki za magonjwa ya ngozi, kliniki za afya ya uzazi, pamoja na mtaalamu wa magonjwa ya wanawake au mkunga wa jadi au dispensali yako.

Vipimo vya VVU vinavyofanyika Noaks Ark

Baadhi ya taasisi zetu hutoa huduma ya vipimo vya haraka vya VVU (dakika 15). www.noaksark.org/hivtest

Pata kituo chako cha kipimo

Klinika Uswidi yote: www.hivtest.nu

Je, una maswali kuhusu VVU (Virusi Vya UKIMWI)?



Wasiliana na Noaks Ark Direkt kwa njia ya simu 020-78 44 40
www.noaksark.org

VVU ni nini?

VVU (Virusi Vya UKIMWI) ni virusi inayosababisha ambukizo ya kudumu na yanayoweza kutibiwa. Mpaka sasa hakuna dawa ya VVU, lakini nchini Uswidi matibabu na huduma ya afya vina ubora wa hali ya juu kiasi kwamba mwathirika wa VVU anaweza kuishi maisha marefu sawasawa na mtu ambaye hajaathirika. Hata hivyo mwathirika wa VVU asipopatiwa matibabu anaweza kuhatarisha maisha na kusababisha UKIMWI. Ndio maana ni muhimu kupimwa VVU ili kuweza kuanza matibabu mapema haraka iwezekanavyo.

Tembelea kurasa zetu za maelezo mtandaoni kwenye tovuti ya:

www.noaksark.org/omhiv

VVU inaambukizwaje?

Hatari ya maambukizi ya VVU kutoka kwa mmoja kwenda kwa mwingine ni kubwa zaidi katika miezi ya mwanzo baada ya kuambukizwa, kabla ya kuanza matibabu. Kipindi hicho kuna kiasi kikubwa cha virusi mwilini, mwenye VVU akiwa hafahamu.

VVU inaweza kuambukiza kupitia tendo la ngono kutokutumiwa kingo kwa njia ya haja kubwa, uke, pamoja na mdomo au kupitia kuchangia vifaa vya kuchomea sindano za dawa na mwathirika. Virusi vinaweza kuambukizwa pia kwa mtoto wakati wa ujauzito, kuzaliwa au kunyonyeshwa.

VVU haviwezi kuambukizwa kupitia mahusiano au mawasiliano ya kijamii.

Mwathirika anapotumia dawa

Siku hizi matibabu ya VVU ni madhubuti kiasi kwamba inawezekana kupunguza kiwango cha virusi mwilini mpaka iwe vigumu kuviona kwa vipimo. Matumizi ya dawa za kupunguza nguvu ya VVU kwa kiwango na utaratibu sahihi, hatari ya maambukizi ya VVU kupitia tendo la ngono hupungua kiasi cha karibu na sifuri.

Mwanamke kumuambukiza mtoto VVU wakati wa ujauzito au uzazi ni ndogo sana iwapo matibabu yataanza kwa wakati mwafaka. Hatari ya maambukizi kupitia kuchangia sindano na jinsi inavyoathiriwa na matibabu haijafahamika mpaka sasa, lakini kwa ujumla inatambulika kuwa matibabu ya VVU yanapunguza kwa kiasi kikubwa hatari ya maambukizi ya VVU.

Jilinde wewe mwenyewe na wengine

Mtu anaweza kuathirika na VVU pasipo kufahamu. Matumizi ya kondomu ni njia nzuri ya kujilinda mwenyewe na wengine dhidi ya VVU pamoja na magonjwa zingine za zinaa. Kamwe usichangie sirinji au sindano na mtu yeyote.

Nenda kapimwe VVU kama huna uhakika na usiogope kumwuliza mwenza wako kimapenzi iwapo ameshapimwa VVU.

Hatari ya kuambukiza au kuambukizwa VVU huongezeka iwapo tayari una maambukizi mengine ya ugonjwa wa zinaa.